# Makubaliano Kati ya Jamii ya Maa na Uingereza, 1904 and 1911


## Shukrani

*Mwandishi wa kwanza:* Ng'ang'a Wahu-Mũchiri

*Waandishi wa pili:* Chao Tayiana Maina and Adrian S. Wisnicki

*Mfasiri:* Mziwanda Banda

*Chapisho*: "Recovering the Histories of Land Treaties in East and Southern Africa"

*Tarehe ya Kuchapishwa:* 2024

*Wachapishaji:* *The Ardhi Initiative* and *One More Voice*

*Mfadhili:* American Council of Learned Societies (ACLS)



*Leseni:* CC BY 4.0



*Rejea (Chicago):* Wahu-Mũchiri, Ng'ang'a; Chao Tayiana Maina; Adrian S. Wisnicki. 2024. "Makubaliano Kati ya Jamii ya Maa na Uingereza, 1904 and 1911." Translated by Mziwanda Banda. In "Recovering the Histories of Land Treaties in East and Southern Africa." *The Ardhi Initiative*; *One More Voice*, solidarity edition. https://onemorevoice.org/pdf/recovering-histories/makubaliano-kati-ya-jamii-ya-maa-na-uingereza.pdf.

# Yaliyomo

Muhtasari....................................................................................................................3
Mahusiano kati ya Ardhi na masuala ya Kikabila na Kiroho............................................3
Historia ya Uhamiaji kuingia Afrika Mashariki.....................................................................5
Maa ni kina nani?.......................................................................................................6
Utoaji wa Kigeni..........................................................................................................7
Maoni ya Wakoloni Wazungu kuhusu Maa.........................................................................8
Kufanya Mkataba.......................................................................................................8
Maswali Yasiyotatuliwa..............................................................................................10

## Muhtasari

Makala haya yanatoa mwongozo wa mada kuu zinazohusu ubeberu wa Wazungu wa karne ya kumi na tisa katika Afrika Mashariki. Miongoni mwa mada mbalimbali, makala haya yanatoa tafakuri ya jumla na kupendekeza matini nyingine za usomaji wa ziada. Kwa jumla, sehemu hizi zinaibua masuala muhimu yanayohusiana na mitazamo ya Afrika Mashariki kuhusu ardhi na kushindwa kwa watawala wa kizungu na wakoloni kutambua na kutumia maarifa ya kiasili.

## Mahusiano kati ya Ardhi na masuala ya Kikabila na Kiroho

*Muhtasari:* Yanajadili mbinu ambazo visasili vya Kiafrika kuhusu kuishi vilisisitiza uhusiano kati ya mazingira na miuja.

*Hapo zamani, zamani za kale, paliishi sungura. Jina lake lilikuwa Dada Sungura. Dada Sungura angecheza mbugani kwa siku nzima, kutembea msituni, kula majani na kuota jua. Jioni, magharibi yalipokaribia, na jua kutua, angeanza kuwa na wasiwasi.*

*Alichukia jioni zilizokuwa na baridi, hata kama alipenda kutumbulia macho nyota na kilimia. Aliishi hivi kwa siku nyingi: mwenye furaha mchana, mwenye baridi nyingi na kukosa raha usiku.*

*Dada Sungura alijiuliza cha kufanya. Alifikiria kwa muda mrefu. Hatimaye, aliazimu kujenga shimo zuri. Ilimgharimu Dada Sungura siku kadhaa kukamilisha shimo hilo, na hatimaye, alifurahia juhudi zake. Shimo lile lilikuwa zuri na lenye joto la wastani usiku. Hakuhisi tena baridi.*

*Kisha, jioni moja, simbajike alikuja hapo. Alizungumza kwa sauti nzuri na tulivu. “Dadangu Sungura,” Simbajike alisema. “Ninaomba unisaidie. Ninahisi baridi sana usiku. Niruhusu niutulize mkia wangu tu kwenye hili shimo lako lenye joto la wastani. Angalau, ikiwa mkia wangu utapata joto, mwili wangu mzima utakuwa sawa tu. Dada Sungura, tafadhali nisaidie.” Dada Sungura aliliwazia hili. Aliogopea kucha za simbajike. Lakini mwishowe, alimkubalia.*

*Usiku ule wa kwanza, simbajike aliuweka mkiwa wake kwenye shimo la Dada Sungura. Usiku uliofuata, simbajike aliuweka mkia wake na miguu yake ya nyuma. Usiku wa tatu, simbajike aliuweka mkia wake, miguu ya nyuma na ya mbele. Wakati uo huo, mkia wa Dada Sungura, miguu yake ya nyuma na ya mbele ilikuwa inaendelea kusukumwa nje ya shimo lile. Baada ya siku tano, simbajike alikuwa amechukua umiliki wa shimo lile naye Dada Sungura alikuwa amekwishasukumwa nje kabisa.*

Hurafa iliyosimuliwa hapo juu inavutia sana kwa utambuzi wake wa kuwepo kwa viumbe ambavyo si binadamu katika nchi za Afrika, hususan Afrika Mashariki, kabla ya uhamiaji wa wanadamu. Uwepo huu wa awali ni muhimu kwa sababu mbili: unahusiana kwa karibu na dhana za kienyeji za asili; kisha unapanga uhusiano wa utunzaji ambapo vitu visivyo wanadamu vinarithisha watu ardhi, ambao wanapaswa kulinda mfumo wa ikolojia kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Hoja inayoshikilia kuwa Wanyama waliishi Afrika Mashariki kabla ya ujio wa wanadamu imerudufiwa kotekote katika masimulizi ya Kiafrika. Dhana za kiasili za umilikaji wa ardhi ni itikadi zilizojikita kwa kina na zimeenea hata katika mazungumzo ya kisasa kuhusu kuishi, kutambulika, na jina. Chimbuko la ni swali muhimu. Neno “nyumbani” lina maana mbalimbali: makazi ya mtu ya sasa (yumkini mjini), mahusiano na ukoo na jamaa (huenda maeneo ya mashambani), n.k.

Dhana za nyumbani zimetumiwa kuunganisha miungano ya lugha anuwai kwa malengo ya kisiasa na kitamaduni. Nyumbani pia limetumiwa kugawa siasa za kitaifa. Tawala za kikoloni, ukiwemo utawala wa Wazungu, ulifuatilia sera ya kugawa na kutawala. Kuzipachika jamii majina ya kikabila ilikuwa mbinu ya kikoloni iliyovunja na kuchelewesha vita dhidi ya ukoloni.

Zaidi ya asili, hurafa iliyo hapo juu inaonyesha uhusiano mzito kati ya mandhari na miuja. Ijapokuwa wanyama wanadhihirika kama viumbe vya asili vya mazingira yasiyo wanadamu, roho za mababu na miungu iliyodhihirika kwa njia mbalimbali zilikuwa, na zingali, kipengele kikuu cha uhusiano wa karibu wa mwanadamu na ardhi katika Afrika Mashariki na sehemu nyinginezo za bara la Afrika.

Mara kwa mara, jamii za kiasili zilipanga maisha yao ya kila siku kwa kuzingatia dhana za kiroho kuhusiana na sifa za topografia. Mathalani, jamii ya Maa ilitekeleza sherehe za kidini kwenye milima mahususi. Jamii nyinginezo zilipanga shughuli za ukulima, uvuvi, na kilimo, pamoja na mitagusano yao na roho za wanyama; kwa sababu hiyo, kwa mfano, wawindaji waliepuka kumwua mnyama ambaye jamii zao zilichukulia kuwa mzimu ama mwenye uhusiano nao katika ukoo wa kiroho.

Mahusiano kati ya wanadamu na miuja yanatoa msingi wa uhusiano wa utunzaji kuhusu ardhi. Kuna imani dhahiri kuwa mababu waliwarithisha walio hai ardhi na urembo wake wote. Kama malipo, wakazi wa sasa wanatekeleza wajibu wa utunzaji, kuhifadhi mfumo wa ikolojia kwa manufaa ya watakaozaliwa baadaye. Walio hai wana majukumu mawili: kuendeleza kumbukumbu za waliotangulia, na kutunza ardhi kwa ajili ya watakaokuja baadaye. Shughuli wafanyazo walio hai katikati ya maisha yao ya kila siku zinalenga kudhihirisha mahusiano kati ya mababu na watakaozaliwa baadaye.

## Usomaji wa Ziada

Gathogo, Julius. 2020. “Settler-Missionary Alliance in Colonial Kenya and the Land Question.” *Studia Historiae Ecclesiasticae* 46 (2): 20.

Musiyiwa, Mickias. 2016. “Shona as a Land-Based Nature-Culture: A Study of the (Re)Construction of Shona Land Mythology in Popular Songs.” In *Natures of Africa: Ecocriticism and Animal Studies in Contemporary Cultural Forms*, edited by F. Fiona Moolla, 49–76. Johannesburg, SA: Wits University Press.

## Historia ya Uhamiaji kuingia Afrika Mashariki

*Muhtasari:* Yanachunguza uhamiaji wa kihistoria wa jamii za kuhamahama katika Afrika Maashariki

Kuna historia pana ya tangu jadi kuhusu uhamiaji katika Afrika Mashariki. Safari za watu katika karne ya ishirini na moja zimejengwa kwenye desturi za mikondo ya uhamaji. Wakati mwingine safari hizi huwa za kujirudiarudia, mara nyingine huwa za kuelekea upande mmoja. Jamii ya Maa ina sifa anuwai. Kundi hilo linajumuisha lugha zinazohusiana kwa karibu kama vile Samburu. Mitazamo mbalimbali ya kitamaduni kutoka Il-Ndorobo, hadi Maa, hadi Samburu inaonyesha kutotulia kama sifa kuu tambulishi ya Maa. Makala haya yanatumia “Maa” kurejelea jamii. Ijapokuwa Maasai ndilo jina lililozoeleka sana, Maa ni sahihi sana, kama maelezo ya watu wanaozungumza lugha ya Maa.

Jamii za Niloti, ambazo Maa ni sehemu yake, zilihamia makao ambayo leo hii ni Sudan, Sudan Kusini, Uhabeshi, Kenya, Uganda na Tanzania kandokando ya Mto Nile. Nyingi za, ijapokuwa si zote, jamii za Niloti ambazo wakati mwingine huwekwa kwenye kundi moja hufanya ufugaji wa kuhamahama. Kiungo cha familia na njia za jumuia za kuishi zimepangwa kwa kuzingatia safari za mara kwa mara kutafuta malisho na maji ya mifugo.

Mtindo wa wakoloni wa ugavi wa ardhi, na majilio ya mifumo ya usimamizi wa ardhi iliyojikita kwenye mali ya kibinafsi, ilimaliza mirathi hii. Nyua, kingo, na mipaka ilivunjavunja sifa asilia za maeneo, yaani, topografia. Kanda za mbuga zilizokuwa wazi zilibadilishwa na kuwa mashamba ya walowezi ya kufugia ng’ombe wa maziwa na mashamba ya mifugo, yaani, ranchi. Sehemu za kunyweshea mifugo maji zilizokuwa katika migunda ya wakoloni iliyoundwa zilikuwa marufuku. Kutokana na mahusiano yaliyokuwa na maana kati ya wanadamu na topografia, ardhi za Kiafrika zinazorejelewa zilichukuliwa kama urithi asili waliojaaliwa. Kinyume na hiyo, tawala rasmi za wakoloni ziliharamisha kupita kwenye ardhi ya mtu bila ruhusa na kuzurura; sera kama hizo ziliipa ardhi umuhimu zaidi – na kuyapokonya mandhari sifa za kiasili zozote za

kitamaduni na kiroho. Kuipa ardhi ya Kiafrika umuhimu zaidi kwa wakoloni, pia hakukutambua mahusiano thabiti kati ya wanadamu na roho zilizoishi kwenye mandhari hayo hayo

Mitazamo ya walowezi ilifasiri vibaya mikondo ya safari za Maa kuwa safari tu zisizo na utaratibu maalum. Kwa kweli, mikondo ya uhamiaji wa wahamahamaji ilishikamana na mikondo ya hali za anga, kuwepo au kutokuwepo kwa vijasumu vya maradhi, na ufaano baina ya wanadamu na wanyama. Jitihada za kupinga ukoloni zilitetea urejeshaji wa upataji ardhi ya kienyeji. Jamii zilizofanya ufugaji wa kuhamahama na/ au kilimo cha kuhamahama zilieleza kwa ufasaha malengo ya kupinga ukoloni kwa ajili ya haki pana za mali asili.

### Usomaji wa Ziada

Hirbeck, I., ed. 1988. “The East African Interior.” In *General History of Africa: (III) Africa from the Seventh to the Eleventh Century*, 297–306. Berkley: California University Press.

## Maa ni kina nani?

*Muhtasari:* Yanajadili utambulisho wa Maa, na sifa yao ya kutotulia

Mitazamo ya umma kuhusu jamii ya Maa inasisitiza mahusiano yao na mifugo. Yapata miaka hamsini iliyopita, tamaduni za Kimaasai zimeonyeshwa sana kama mojawapo ya hifadhi za mwisho za “kweli” za Afrika – safi na zisizokengeuka. Mitazamo yote ina umuhimu wake na tena ina makosa. Hali ya *Il-Ndorobo*, neno la Maa linalomaanisha “watu wasio na ng’ombe” linaonyesha nafasi muhimu ya mifugo katika maisha ya Maa. Ng’ombe humaanisha chakula, namna ya kuishi, mpango wa kustaafu, akiba ya dharura, na hadhi katika jamii. Licha ya haya, uanuwai uliomo miongoni mwa wazungumzaji wa lugha ya Maa unapisha nafasi ya jamii – kama vile zile zilizo karibu na Arusha katika Tanzania ya leo – zinazojitambulisha kama Maa asili, ijapokuwa hukwepa ufugaji na kufanya kilimo-mseto cha mimea kwenye maeneo ya mwinamo ya Mlima Kilimanjaro.

Pamoja na mawazo mepesi ya kuhusisha Maa na ng’ombe, kuna pia uchanganuzi wa kimazungumzo wa Maa kuchangamana na jamii nyingine hasa Gikuyu na Kamba. Kuna mawazo ya kweli kinzani yanayoonyesha Maa kama watu wenye mtazamo finyu wa mumo humo tu na pia kama wenye mtazamo mpana wa kidunia.

Maoni haya yanayokinzana yanaakisi athari za safari na usimilishaji kwa muundo wa jamii katika Afrika Mashariki. Hali ya Il-Ndorobo kutokuwa na ng’ombe, inatambua

uwezekano wa msuguano wa utambulisho wa Maa. U-Maa u kwenye mfululizo wa mabadiliko kila wakati – si thabiti. Ikolojia asili ya jamii hii, hususan majina mengi ya mahali ambayo yamedumu mpaka topografia za leo, inadhihirisha mwingiliano wa Maa na mazingira yao. Uhamiaji wa jamii za Kiafrika uliunda hali kwa minajili ya utambulisho wa jamii zilizoishi bila kutulia bali katika mabadiliko kila wakati.

### Usomaji wa Ziada

Chao, Tayiana Maina. 2023. "Many Places in Nairobi and Wider Kenya Derive Their Origins from Maasai Words." *X*. February 10, 2023.

Thompson, Leonard. 2000. *A History of South Africa*. 3rd ed. New Haven: Yale University Press.

## Utoaji wa Kigeni

*Muhtasari:* Yanachunguza ubeberu wa Wazungu na hamu yao kwa Waafrika na mali asili zao

Mahusiano ya kujirudiarudia yaliyoelezwa hapo juu, ambapo walio hai huomba kwa mizimu kwa niaba ya watakaozaliwa, yanapendelea matumizi endelevu ya ardhi tofauti na utoaji kupindukia. Athari ya kigeni kwenye ardhi ya Kiafrika, ikiwemo Afrika Mashariki, imependelea mara kwa mara uzalishaji mali ghafi kupitia michakato inayoweka shinikizo isiyostahili kwenye mazingira. Kihistoria, kwa mfano, utoaji wa pembe za ndovu kutoka kwenye mbuga za Kiafrika ulisababisha kupungua sana kwa idadi ya ndovu.

Zaidi ya hayo, katika karne ya kumi na nane na kumi na tisa, mikondo ya utoaji wa pembe za ndovu ulitegemea na ulijikita kwa kuwafanya Waafrika watumwa. Masoko ya Waafrika watumwa katika nchi za Marekani, Ghuba, na kotekote kujulikanako sasa kama Mashariki ya Kati, yalichochea kuundwa kwa njia mbili za biashara: watumwa – ambao wangeuzwa kwa faida – kubeba pembe za ndovu kutoka bara hadi pwani. Pembe za ndovu na bidhaa zake zilikuwa kama kitegauchumi cha pili – ijapokuwa zilikuwa zenye kuleta faida kubwa.

Biashara ya pembe za ndovu ilizaliwa na kuzidishwa nguvu na uundaji wa masoko ya bidhaa zilizotengezwa na Wazungu Afrika. Shanga za vioo, nguo za Marekani, na bunduki na risasi zilitolewa na Wazungu na Waarabu waliozuru. Bidhaa hizi zilitumika kama pato la ushuru kwa jamii za kienyeji na zikawapa Wazungu ridhaa ya kufika hadi maeneo ya ndani ya bara la Afrika bila vizuizi. Kama malipo, wasafiri wa Kizungu walitarajiwa wapewe ulinzi, chakula na wapagazi. Muda baada ya muda, ushindani wa

Wazungu uliofuata kuwania utiifu wa jamii za Afrika ulifikia hali kama mashindano ya mnada. Kundi la Wazungu lililojiweka kwenye nafasi bora kutoa maficho ya bidhaa lilishinda ushawishi na kukubaliwa huku wengine wote wakiambulia patupu.

Picha ya maonyesho kwenye Makavazi ya Kitaifa ya Kenya. Picha: NWM Leseni: CC4

### Usomaji wa Ziada

Maughan-Brown, David. 1985. *Land, Freedom & Fiction: History & Ideology in Kenya*. London: Zed Books.

## Maoni ya Wakoloni Wazungu kuhusu Maa

*Muhtasari:* Yanachunguza dhana za kikoloni dhidi ya zile za kiasili kuhusu usimamizi

Mfalme wa Uingereza alikuwa siku zote akimtafuta “mfalme” wa Maa. Kuhusisha dhana za Wazungu kuhusu mamlaka na usimamizi kwenye jamii asili za Kiafrika kulidhihirika kuwa jitihada isiyo na mafanikio.

Isitoshe, badala ya kufanya tathmini wazi ya shughuli za maisha za Maa za wanaume dhidi ya zile za wanawake katika jamii, Wazungu walileta mtazamo wa jinsia kutoka mitazamo mingine potovu ya wanawake weusi kutoka bara Hindi. Matamshi ya Wazungu wa enzi ya Malkia Victoria kuhusu kaida za kijinsia yalifasiri visivyo majukumu ya wanawake katika utamaduni wa Maa.

Upendelevu wa wakoloni kwa ajili ya miundo mbinu halisi na mfanano wa maisha ya mjini uliwafumba macho walowezi Wazungu wakakosa kuona jinsi jamii za Maa zilivyosimamia makazi yao. Umilikaji, kwa mujibu wa sera ya kikoloni, ulihitaji kuzingira nyua, mali ya kibinafsi na hati miliki.

### Usomaji wa Ziada

Dinesen, Isak. 1937. *Out of Africa*. New York: Modern Library.

## Kufanya Mkataba

*Muhtasari:* Yanachunguza jinsi mkataba wa kikoloni ulivyotumiwa kama kifaa cha kibeberu cha kutawala na kutenga ardhi

Jamii asili za Kiafrika zilifanya miungano ya kisiasa kupitia kwa biashara, ndoa za kati ya makabila, na “upangaji” wa watoto. Desturi hizi mbili za mwisho zilisisitiza mtazamo ulioegemea ukoo kwa ajili ya kupanua ushawishi wa kisiasa.

Tofauti na hiyo, desturi za kufanya mkataba za kikoloni zilipendelea mikataba mbali mbali ya maelewano na madola mahususi ya Kiafrika kwa sababu mbalimbali. Kwa mtu yeyote, upanuzi wa milki ulikuwa mchakato mgumu na usiotabirika. Wakati wowote kama ingewezekana, watawala wa kikoloni walidai mapato kiasi – aghalabu yaliyotolewa kama mikataba ya ardhi na makubaliano na jamii asili mahususi.

Desturi za wakoloni pia zilipendelea mikataba mbali mbali. Ilimpendelea Mfalme wa Uingereza kuwa jamii katika Afrika Mashariki hazikuungana na kupinga ubeberu. Mikataba iliyofanywa na watu asilia mbalimbali ilijumuisha kukubali kutegemea hali mbalimbali, jinsi jamii mbalimbali zilivyotetea mapendekezo yao. Kwa mfano, Wazungu walitambua utawala wa Waswahili kandokando ya Bahari ya India huku wakikana kujitawala kwa walioishi bara.

Hatimaye, ushindani wa Wazungu kupata milki ulisababisha ufanyaji wa mikataba mbali mbali. Katika matukio kadhaa, serikali mbili za Kizungu zingefanya mikataba na vikundi tofauti tofauti katika jamii moja. Njia hii ya kugawa ilimaliza nguvu upinzani wa Waafrika dhidi ya wakoloni walioingilia ardhi yao.

Mikataba na sheria za ardhi za kikoloni zilipata msingi wake kutokana na ugavi wa ardhi kwa walowezi Wazungu kwa sababu Waafrika “hawakuwa wakiitumia.” Hiki kilikuwa kisingizio cha kutetea hatua yao ya uvamizi. Kiasilia, dhana za Wazungu za matumizi/umilikaji wa ardhi zinajikita kwenye nia za kibepari, yaani, ili kuthibitisha kuwa ardhi ina mwenyewe, mtu anapaswa kuzalisha mapato au kupata faida ya kiuchumi kutokana na ardhi hiyo. Kwa hiyo, kwa kinaya, mlowezi mmoja kumiliki na kulangua makumi ya maelfu ya ekari ilikuwa ithibati ya umilikaji ilhali jamii nzima ya watu wanaotumia ardhi kwa malengo yaliyofungamanishwa na mifumo ya kibiashara ya kienyeji na uzalishaji haikuwa ithibati tosha.

Kutokana na hali hii, mitazamo ya kiasilia ya thamani ya ardhi ilipuuzwa, huku mitazamo ya Wazungu ya matumizi ya ardhi ikipendelewa. Mikataba inaficha sawia na kufichua visingizio hivi; hususan katika muktadha wa mapatano ya 1911 ambapo kimsingi, Wazungu walitwaa ardhi iliyopewa Wamaasai chini ya mapatano yao ya 1904 (Lenana et al. 1914) kwa kuwa ghafla waligundua thamani yake kiuchumi. Mpaka leo, idadi kubwa ya ardhi hizi imesalia chini ya usimamizi wa Waingereza na familia za Wazungu zenye ukwasi kwa kisingizio cha uhifadhi wa wanyamapori.

Mzozo wa kisheria wa 1913 ambapo Wamaasai walipinga mikataba hiyo unatoa mfano thabiti wa jamii asilia kutumia mbinu za Kizungu za kisheria kupinga hatua za Wazungu za ukiukaji wa sheria. Kimsingi, hakuna jinsi Wamaasai wangeshinda kesi ambayo

walifanyiwa hila toka mwanzoni. Hata hivyo, mapambano ya kisheria yanaakisi nguvu asilia, muundo wa kijamii, mifumo mbalimbali ya jitihada za kupinga ukoloni, na athari za ukoloni za kudumu katika asasi za Kiafrika baada ya ukoloni.

Mikataba na kesi zilizofanyika mahakamani bila mafanikio ilisababisha kipindi cha uhamaji wa lazima. Lotte Hughes (2023) anaeleza kupitia maandishi kuhusu kuunganisha kwa hesabu za historia za masimulizi zinazochora picha ya hali mbaya sana ya familia za Maa: kufurushwa kwenye ardhi zao, magonjwa, njaa, kupoteza mifugo na vifo. Masimulizi haya yanatoa mtazamo wa kibinafsi katika matokeo ya mikataba. Mikataba ni zaidi ya mapatano yaliyotiwa sahihi na watu wenye ushawishi wa kubadilisha historia – ni nyenzo zinazosababisha mateso makubwa na ya kutia kiwewe, na kuacha alama za kudumu katika akili na kumbukumbu za watu.

## Usomaji wa Ziada

Caulker, Tcho Mbaimba. 2009. *The African-British Long Eighteenth Century: An Analysis of African-British Treaties, Colonial Economics, and Anthropological Discourse*. Lanham, MD: Lexington Books.

Hughes, Lotte. 2023. "2023 Marks 110 Years Since the Maasai Case 1913: Does It Still Matter?" *The Elephant* (blog). September 7, 2023.

Lenana, et al. (1914) 2023. "[Treaty/Agreement of 10 and 15 August 1904]." Edited by Ng'ang'a Wahu-Mũchiri and Adrian S. Wisnicki. In *One More Voice*, solidarity edition; *The Ardhi Initiative*.

Mugambwa, John. 1987. "Treaties or Scraps of Paper? A Second Look at the Legal Character of the Nineteenth Century British/African Colonial Agreements." *The Comparative & International Law Journal of Southern Africa* 20 (1): 79–93.

Segi, et al. (1914) 2023. "[Teaty/Agreement of 4 and 13 April 1911]." Edited by Ng'ang'a Wahu-Mũchiri and Adrian S. Wisnicki. In *One More Voice*, solidarity edition; *The Ardhi Initiative*.

## Maswali Yasiyotatuliwa

Historia ya ufanyaji mikataba katika Afrika Mashariki bado haijaandikwa na inaibua maswali kadhaa: Kwa kuwa Wazungu walinyang'anya eneo la nchi ambayo sasa ni Kenya, je, kulikuwa na haja yoyote kufanya mkataba tofauti na Wamaasai? Katika kujitokeza polepole kwa milki, je, ni Mkataba wa Maasai wa 1904 wa kwanza kufanywa sheria? Kama sivyo, je, ni mikataba gani mingine tusiyoifahamu? Vilevile, kwa kuwa Wamaasai walikuwapo katika Afrika Mashariki ya Uingereza na Afrika Mashariki ya

Ujerumani, je, hizi serikali mbili za kikoloni zilihusiana vipi na jamii ya Maa? Kwa mfano, je, mkataba wa Waingereza na Maa ulirudufiwa na Wajerumani ama je, ukinzani wa ndani wa ushindani kati ya Wazungu ulizaa mtazamo wa kutowiana? Hatimaye, tunatoaje uhuru wa tasnia ya uhifadhi wa wanyamapori kwa vile ina uhusiano na historia ya wizi wa ardhi? Nchini Kenya, mashamba mengi ya hifadhi (k.v katika eneo la Laikipia) yalitwaliwa kutoka kwa jamii asilia kupitia kwa Mikataba ya 1904 na 1911. akala haya yanapendekeza jinsi wasomi na wataalamu maarufu katika nyanja mbalimbali wanaweza kutatua maswali haya.